Bwana Yesu, naja, naja.

4. Hivi nilivyo kipofu,
Maskini na mpungufu,
Wewe Umtimilifu;
Bwana Yesu, naja.

Edit with WPS Office

MAOMBI

5. Hivi nilivyo nitwae,
Sithubutu kushangaa,
Wewe hutanikataa,
Bwana Yesu, naja, naja

6. Hivi nilivyo mapenzi,
Yamenipa njia wazi;
Mali na yote ni yako,
Bwana Yesu, naja, naja.

NI WEWE MCHUNGA MWEMA

JESUS TENDER SHEPHERD, HEAR ME

NT 384 Jesus, tender shepherd OT 268 G

81.

Ni wewe mchunga mwema,
Nami kondoo wako;
Hivi nalala salama,
Ni mkononi mwako.

2. Nimelindwa leo kuchwa,
Hofu kwangu hapana;
Nimevikwa, nimelishwa,
Nakushukuru Bwana.

3. Nisamehe dhambi zangu,
Wabariki rafiki;
Nichukue, Mungu wangu,

Edit with WPS Office

Kwako, nikifariki.

MAOMBI

NA UNI MEGEE MKATE HAI

BREAK THOU THE BREAD OF LI FE

NT 713 Lathbury OT 719 E Flat

82.

Na unimegee, Mkate hai,
Kama ulibyomega zamani,
Ninakutafuta. Ewe Bwana,
Roho yangu yakutaka sana.

2. Na unimegee Mkate hai,
Neno lako likae moyoni;
Mawazo ya ndani, yawe safi,
Niongoze daima, Mwokozi.

3. Neno lako Bwana, nilione,
Ujumbe wako niandikie;
Tushirikiane na upendo,
Unitilie sura yako.

Edit with WPS Office

MAOMBI

USI NI PI TE MWOKOZI

PASS ME NOT, O LOVI NG SAVI OR

NT 346 My humble Cry NT 347 Pass me not OT 240 G

83.

Usinipite Mwokozi,
Unisikie,
Unapozuru wengine,
usinipite.

Yesu, Yesu, unisikie,
Unaopozuru wengine,
Usinipite.

2. Penye kiti cha rehema,
Nipate nafuu,
Napiga magoti kwako,
Unisamehe.

3. Sina la kuaminia,
Rohoni mwangu,
Niponye jeraha zangu,
Kwa neema yako.

Edit with WPS Office

MAOMBI

YESU KWETU NI RAFIKI

WHAT A FRIEND WE HAVE IN JESUS

NT 340 Blaenwern NT 438 Hyfrydol NT

84.

Yesu kwetu ni rafiki,
Huambiwa haja pia;
Tukiomba kwa Babaye,
Maombi husikia;
Na sisi twajikosesha,
Twajitwika vibaya,
Kwamba tulimwomba Mungu,
Dua atasikia.

2. Una dhiki na matakwa,
Una mashaka pia?
Haifai kufa moyo,
Dua atasikia;
Hakuna mwingine mwema,
Wa kutuhurumia,
Atujua tu dhaifu,
Maombi asikia.

3. Je, hunayo hata nguvu,
Huwezi kuendelea?
Ujapodharauliwa,
Ujaporushwa pia;
Watu wakikudharau,
Wapendao dunia,
Hukushika mikononi,
Dua atasikia.

Edit with WPS Office

MAOMBI

ZI KO BARAKA KWA WI NGI

THERE SHALL BE SHOWERS OF BLESSI NG

NT 456 Shower s of blessing OT 653 B Flat

85.

Ziko Bar aka kwa wingi
Mungu ameahidi,
Wako wakat i war aha,
Toka kwake Mwokozi.

Bar aka kwa wingi,
Hizo t waomba kwako,
Sasa t wapat a kidogo,
Nyinyi ndizo t ut akazo.

2. Ziko Bar aka kwa wingi,
Za kut uj aza t ena,
Uvumo t unasikia,
Ukit oka mbinguni.

3. Ziko Bar aka kwa wingi,
Hebu Bwana, t ut olee,
Kama umande kwa nyasi,
Ee Bwana, Ut unyweshee.

4. Ziko Bar aka kwa wingi,
Sasa t waombea kwako,
Leo t waj a kuungama,
Yesu, sikia kilio.

Edit with WPS Office

MAOMBI

ATI KUNA MVUA NJEMA

LORD I HEAR OF SHOWERS OF BLESSI NG

NT 369 Even me OT 265 G

86.

Ati kuna mvua njema,
Yenye yenye neema;
Watu wanaona vyema,
Bwana, uninyeshee;
Na mimi, na mimi,
Bwana uninyeshee.

2. Usinipite, Mwokozi,
Nina dhambi moyoni,
Rehema zako huduma,
Bwana unisamehe;
Na mimi, na mimi,
Bwana uninyeshee.

3. Usinipite, Mwokozi,
Niwe nawe daima,
Natamani kukuandama,
Bwana nihurumie;
Na mimi, na mimi,
Bwana uninyeshee.

4. Umekasirika kwangu;
Nina macho mazito,
Kwa kupenda ulimwengu,
Bwana, uniokoe;
Na mimi, na mimi
Bwana uninyeshee.

Edit with WPS Office

MAOMBI

5. Usinipite, Mwokozi,
Mpaji wa uzima,
Nawe shahidi wa wema,
Bwana, nipe uwezo;
Na mimi, na mimi,
Bwana uninyeshee.

WAKATI WANGU KUOMBA

SWEET HOUR OF PRAYER

NT 66 Sweet hour of prayer OT 44 D

87.

Wakati wangu kuomba
Umenialika kusali,
Nimsihi Mungu mwenyezi,
Anitulize kwa mapenzi;
Nyakati za shaka nyingi,
Nimepata ufadhili,
Kwa wewe nitangojea,
Ewe, wakati wa kuomba.

2. Wakati wangu kuomba,
Umenileta furaha,
Pamoja nao wenzangu,
Nashirikiana na Mungu,
Mahali hapa nikae,
Uso wa Mungu nimwone;
Kwako nitakungojea,
Ewe, wakati wa kuomba.

Edit with WPS Office

MAOMBI

3. Wakati wangu kuomba,
Mabawa yako hunishika,
Kwa Yesu aliye kweli,
Aningoja kubariki;
Tangu alinialika,
Nimwamini kwa hakika,
Kwa wewe nitangoja,
Ewe, wakati wa kuomba.

UONGOZI NA FARAJA

MAPENZI MEMA YA MUNGU

THOU HIDDEN LOVE OF GOD, WHOSE HEIGHT

NT 487 Thou shepherd of Israel OT 206 G

88.

Mapenzi mema ya Mungu,
Yasiyotambulika.
Ndiyo mfano wa mbingu,
Kwa ukubwa, na upana;
Natamani kuyajua,
Moyo upate nitua.

2. Natafatuta raha asana,
Na ilipo sipajui;
Natafuta, sikuona,
Roho yangu haitui,
Ngawa situlii kwako,

Edit with WPS Office

Nipumzike uliko.

UONGOZI NA FARAJA

3. Je, pana kitu kwangu,
Nilichotia moyoni,
Usichokipenda Mungu?
Nami sipati amani;
Kitoe Bwana kabisa,
Moyo uwe wako sasa.

4. Nisiwe mimi huishi,
Ila Yesu ndani yangu,
Tamaa zangu haziishi,
Usipoziua Mungu;
Nisione kitu kwamwe,
Nisitake, ila wewe.

5. Kila dakika nivute,
Unitenge na dunia;
Wewe Bwana umeniita,
Nami sasa nachagua,
Niandame sautiyo,
Nikaonje mapenziyo.

AHADI YA MUNGU NZURI

PRECIOUS PROMISE GOD HAS GIVEN

NT 429 Bethany NT 379 I will guide thee OT 255 G

89.

Ahadi ya Mungu nzuri,
Atakufikiliza,
Siku zote za safari,
Yeye ‘tatuongoza,

Edit with WPS Office

UONGOZI NA FARAJA

Yeye Mungu, kiongozi,
Jicho lake liko juu,
Kwa wake uangalizi,
Sisi tumwandame tu.

2. Ukijaribiwa sana,
   Kwako kukiwa giza,
   Kumbuka neon la Bwana,
   "Mimi 'takuongoza".

3. Mashaka yakikuja,
   Mambo usiyoweza,
   Jua ukimwamania,
   Yeye 'takuongoza.

4. Siku zako chache tena,
   Punde utamaliza;
   Kumbuka neon la Bwana,
   "Mimi 'takuongoza.

BWANA UPEPO WAVUMA
MASTER THE TEMPEST IS RAGING

90.

Bwana, upepo wavuma,
Wimbi lina ghadhabu;
Wingu hili linanguruma,
Bandari si karibu;
Hali yetu hufikiri?
Kwani kulala, Bwana?
Twafa, maji yawe ni kaburi?
Wokovu, la hapana?

Edit with WPS Office

UONGOZI NA FARAJA

Pepo na mawimbi vyasikiza,
Tulia, tulia,
Kama ukali wa bahari,
Wanadamu, pepo, na shetani,
Mawimbi yapateje kuumiza,
Chombo kilicho na Yesu Bwana?
Mambo pia yamsikiza,
"Tulia, tulia"
Mambo pia yamsikiza,
Hutulia.

2. Bwana nimezima moyo,
Hamu yanizidi tu,
Uniokoe nakuomba,
Nafa na udhia huu,
Dhambi nyingi na uovu,
Zitanizamisha,
Bwana wangu upesi, ni wewe,
Utakayenitosha.

3. Sasa hofu isha kwisha,
Ni shwari baharini,
Lang'ara tena jua letu,
Rohoni kuna shwari;
Kaa name, Ewe Bwana,
Isiwe mimi tu!
Nami nitafika bandarini,
Ng'ambo ndiko na nafuu.

Edit with WPS Office

UONGOZI NA FARAJA

BWANA YU MCHUNGAJI WANGU

THE LORD IS MY SHEPHERD

NT 115 My shepherd NT 82 Crimond OT 561 F

91.

Bwana ni mchungaji wangu,
Hunilaza chini;
Kwa malisho, ya majani,
Huniongoza mimi.

2. Nafsi yangu huhuisha,
Ananitembeza,
Njiani mwake, kwa haki yake,
Katika jina lake.

3. Nijapopita bondeni,
Mwisho wa maisha,
Sitaogopa, baba lolote,
Wewe upo na mimi.

4. Wema wako na fadhili,
Vitanifuata,
Katika nyumba, yake Mungu,
Kutakua makao.

Edit with WPS Office

HUNI ONGOZA MWOKOZI

HE LEADETH ME O BLESSED THOUGHT

NT 21 He leadeth me OT 46 D

92.

Huniongoza Mwokozi,
Ndipo nami hufurahi
Niendapo pote hapo,
Ataniongoza papo.

Kuongoza, hunishika;
Kwa mkono wa hakika;
Nitaandamana naye,
Kristo aniongozaye.

2. Pengine ni mashakani,
Nami pengine rahani;
Niradhi, ijayo yote,
Yupo name siku zote.

3. Mkono akinishika,
Kamwe sitangung'unika;
Atakachonilete a,
Nitayari, kupokea.

4. Nikiisha kazi chini,
"Takwenda huko mbunguni,
Nako nitamtukuza,
Kristo aliyeongoza.

Edit with WPS Office

UONGOZI NA FARAJA

IBADA ITUPAYO
WALK IN THE LIGHT

93.

Ibada itupayo,
Mwangaza, mwangaza,
Furaha ndiyo tamu,
Kwa Mungu Bwana.

Twenende mwangani, mwangani,
Twenende mwangani,
Kwa Mungu Bwana.

2. Ibada hulete a,
Mangaza, mwangaza,
Faraja tukiitwa,
Kwa Mungu Bwana.

3. Furaha kwake kule,
Mwangaza, mwangaza,
Huduma kwa milele,
Kwa Mungu Bwana.

4. Mungu awe rafiki,
Mwangani, mwangani,
Uheri haukomi,
Kwa Mungu Bwana.

Edit with WPS Office

KAA NAMI, NI USIKU TENA

ABIDE WITH ME

NT 520 Emerso NT 522 Sunset NT 517 Abide with me OT 323 E Flat

94.

Kaa name, ni usiku tena,
Usiniache gizani Bwana!
Msaada wako haukomi,
Niko peke yang, kaa name.

2. Siku zetu hazikawii kwisha,
Sioni la kinifurahisha;
Hakuna ambacho hakikomi,
Usiye na mwisho, kaa name.

3. Nina haja nawe kila saa,
Sina mwingine wa kunifaa;
Mimi nitaingozwa na nani,
Ila wewe? Bwana, kaa name.

4. Sichi neon uwapo karibu;
Nipatalo lote, si taabu;
Kifo na kaburi haviumi;
Nitashinda kwako kaa name.

5. Nilalapo nikuone wewe,
Gizani mwote nimulikiwe;
Nuru za mbinguni hazikomi,
Siku zangu zote kaa name.

Edit with WPS Office

UONGOZI NA FARAJA

KARIBU NA WEWE

NEARER MY GOD, TO THEE

NT 187 Horbury NT 190 Nearer my God to thee OT

95.

Karibu na wewe,
Mungu wangu;
Karibu Zaidi,
Bwana wangu;
Siku zote niwe,
Karibu na Wewe;
Karibu Zaidi,
Mungu wangu.

2. Mimi nasafiri,
Duniani,
Pa kupumzika,
Sipaoni,
Nilalapo niwe,
Karibu na Wewe,
Karibu Zaidi,
Mungu wangu.

3. Yote unipayo,
Yanivuta;
Pa kukaribia,
Na nielekezwe;
Karibu na Wewe,
Karibu Zaidi,
Mungu wangu.

Edit with WPS Office

4. Na kwa nguvu zangu,
Nikusifu,
Mwamba, uwe maji,
Ya wokovu;
Mashakani niwe,
Karibu na Wewe,
Karibu Zaidi,
Mungu wangu.

KWA IMANI YANGU

MY FAITH LOOKS UPTO THEE

NT 216 Light NT 215 Harlan OT 367 E Flat

96.

Kwa Imani yangu,
Nitakutumaini.
Peke yako;
Nisikie sasa,
Bwana, nitakase,
Ni wako kabisa,
Tangu leo.

2. Nipe nguvu pia,
Za kusaidia,
Moyo wanfgu;
Ulikufa Wewe,
Wokovu nipewe,
Nakupenda Wewe,
Bwana wangu.

Edit with WPS Office

UONGOZI NA FARAJA

3. Hapa nnazunguka
Katika mashaka,
Na matata;
Palipo na giza;
Utaniongoza,
Hivi nitaweza;
Kufuata.

MAISHA NDIYO SAFARI

BY THE PATHWAY OF DUTY

NT 448 The pathway of duty OT 790 G

97.

Maisha ndiyo safari,
Iendayo mbinguni,
Tuna haja kuongozwa,
Tuna haja ya nuru;
Iko giza duniani,
Ziko hatari nyingi,
Yesu ndiye nuru yetu,
Nuru ya ulimwengu.

Tukienda na Yesu,
Tunaenda kwa nuru,
Tukienda na Yesu,
Tutafika mbinguni.

Edit with WPS Office

UONGOZI NA FARAJA

2. Shetani adui yetu,
Yeye yuko karibu,
Hujaribu kutushinda,
Na kuharibu moyo,
Amewadanganya wengi,
Wengi hushindwa naye,
Lakini tusife moyo,
Hatatushinda sisi.

3. Yesu yu pamoja nasi,
Tusimhuzunishe,
Kwa kukosa kumfuata,
Au yale yasiyofaa;
Ni Yeye anayeweza,
Kuongoza salama,
Na tuongoze gizani,
Twende nuruni mwake.

MBELE NI NAENDELEA
I'M PRESSING ON THE UPWARD WAY

98.

Mbele ninaendelea.
Ninazidi kutemebea;
Maombi uyasikie,
Eh Bwana, unipandishe.

Ee Bwana, uniinue,
Kwa Imani nisimame,
Nipande milima yote,
Ee Bwana, unipandishe.

Edit with WPS Office

2. Sina tamaa nikae,
Mahali pa shaka, kamwe;
Hapo wengi wanakaa,
Kuendelea naomba.

3. Nisikae duniani,
Ni mahali pa shetani;
Mat azamia mbinguni,
Nit afika na Imani.

4. Nataka nipandishwe juu,
Zaidi yale mawingu,
Nit aomba nifikishwe,
Ee Bwana, unipandishe.

MSINGI IMARA ENYI WA KWELI

HOW FIRM A FOUNDATION

NT 566 No never alone NT 569 Dt. Denio OT 684

99.

Msingi imara, enyi wa kweli,
Umekwisha pigwa, kwa neon hili,
Aongoze lipi? Mhayo pia,
Kwa Yesu mliomkimbilia.

2. Usifanye hofu,
Ndimi Mungu wako, nikuwezeshe,
Nit akupa nguvu, thabiti mno,
Nikuinue kwa kono wangu.

Edit with WPS Office

3. Utakapovuka, maji ya giza,
Mito ya mashaka, nitapunguza,
Nitakua nawe hatua zote,
Nikuinue kwa mkono wangu.

4. Utakapopishwa, ndani ya moto,
Nguvu nitakupa, upate pato;
Hutekatezwi, ila taka zako,
Na zitasalia dhahabu zako.

MSINGI WA KANISA

THE CHURCH'S ONE FOUNDATION

NT 246 Aurelia OT 189

100.

Msingi wa kanisa,
Ndiye Yesu Bwana;
Kiumbe kipya chake,
Alipemda sana;
Kutaka itafuta,
Alishuka chini,
Naye kwa hoja kwake,
Akafa mtini.

UONGOZI NA FARAJA

Edit with WPS Office

2. Ina kila kabila,
Kisha ndiyo moja;
Wokovu wake una,
Mwokozi mmoja;
Uzazi ni umoja,
Ni moja Imani,
Chakula ni kimoja,
Moja tumaini.

3. Watu hustaajabu,
Kwa mashaka yote,
Yaipatayo nje,
Hata ndani wote;
Ila watakatifu,
Huomba, wakikesha
Usiku ni kilio,
Asubuhi raha.

4. Mashaka na taabu,
Hata vita vyake,
Vyangoja matimizo,
Ya amani yake,
Ndipo kwa macho yetu,
Tuone utukufu,
Kanisa ya kushinda,
Istarehe juu.

UONGOZI NA FARAJA

Edit with WPS Office

5. Nayo huungamana,
Na Mwenyezi Mungu,
Chini hushirikiana,
Na watu wa mbingu;
Tupe neema, Bwana
Na wao tukae,
Waliotangulia,
Pamoja na Wewe.

MUNGU, BABA YANGU, U MWAMINIFU

GREAT IS THY FAITHFULNESS
NT 657 Great is thy faithfulness

101.

Mungu Baba yangu, U Mwaminifu,
Hakuna geuzo ndani yako,
Hubadiliki wewe ndiwe sawa,
Jana, leo na siku zijazo.

Wewe Mwaminifu, Wewe Mwaminifu,
Kila siku fadhili napewa;
Vitu vyote ninavyo umenipa,
Wewe Mwaminifu, Kwangu Bwana.

UONGOZI NA FARAJA

Edit with WPS Office

2. Na viumbe vyote,
Hulingamana,
Kuonyesha utukufu wako,
Jua, na mvua, mwezi tena nyota,
Hulishuhudia pendo lako.

3. Samaha la dhambi, tena amani,
Hizi zote ni Baraka zako;
Nguvu zako, zitadumu milele,
Nimebarikiwa sasa kwako.

MUNGU MSAADA WETU

O GOD, OUR HELP IN AGES PAST.

NT 127 St. Ann OT 98 C

102.

Mungu Msaada wetu,
Tangu miaka yote,
Ndiwe tumaini letu,
La zamani zote.

2. Kivuli cha kitui chako,
Ndicho ngome yetu,
Watosha mkono wako,
Ni ulinzi wetu.

UONGOZI NA FARAJA

3. Kwanza havijakuwako,

Edit with WPS Office

Nchi na mlima,
Ndiwe Mungu; chini yako,
Twakaa salama.

4. Miaka elfu ni kama,
Siku moja kwako;
Utatulinda daima,
Tu wenyeji wako.

5. Ila wewe, Mungu wetu,
Ndiwe wa kudumu;
Ndiwe bora, ngome yetu,
Twakaa dawamu.

NAAMINI, AMINI

SIMPLY TRUSTING EVERYDAY.
NT 299 Trusting as the moments fly OTG

103.

Naamini – amini,
Nikiwamo dhiki;
Kwamba Imani si kuu,
Namwamini Yesutu.

Niwapo hai chini,
Naamini – amini,
Hata niwasili juu,
Humwamini Yesutu.

UONGOZI NA FARAJA

2. Roho yake kama taa,

Edit with WPS Office

Ndani yangu yang'ara,
Nami sikwai mgumu,
Namwamini Yesu tu.

3. Wakati wa kufaa,
Na mwingine wa shida,
Nijapokuta makuu,
Namwamini Yesu tu.

4. Namwamini kila saa,
Dakika zisizokaa,
Kwa madogo na makuu,
Namwamini Yesu tu.

NADUMU KWA AHADI ZAKE MFALME

STANDING ON THE PROMISES

NT 797 Standing on the promises

104.

Nadumu kwa ahadi zake Mfalme,
Yesu asifiwe kwa siku zote;
Nitamwimbia sana Atukuzwe,
Kudumu kwa ahadi zake.

Dumu, dumu
Nadumu kwa ahadi za Bwana Mungu,
Dumu, dumu,
Nadumu kwa ahadi za Mungu.

UONGOZI NA FARAJA

2. Nadumu kwa ahadi, sina shaka,
Ahadi zisizokosa kabisa,

Edit with WPS Office

Kwa neon lake Mungu, nitashinda,
Kudumu kwa ahadi zake.

3. Nadumu kwa ahadi, nafahamu,
Nina utakaso mkamilifu;
Kudumu kwa uhuru wake Yesu,
Kudumu kwa ahadi zake.

4. Nadumu kwa ahadi zake Kristo,
Kwa milele nimefungwa na pendo,
Nitashinda kwa upanga wa Roho,
Kudumu kwa ahadi zake.

NAMWANDAMA BWANA KWA ALI LONENA

WHEN WE WALK WITH THE LORD
NT 586 Trust and obey OT 754 F

105.

Namwandama Bwana, kwa alilonena,
Njia yangu huning'azia,
Nikimridhisha, atanidumisha,
Niamini nitii pia.

Mwamini, mtii halisi,
Ni kupata furaha,
Kwake Yesu Bwana.

UONGOZI NA FARAJA

2. Giza sina kwangu. wala hata wingu,

Edit with WPS Office

Yeye mara huviondoa,
Woga wasiwasi, sononeko basi,
Niamini nitii pia.

3. Masumbuko yote, Sikitiko lote,
Kwa mapenzi hunilipia;
Baa, dhara, dhiki, vivyo hubariki,
Niamini nitii pia.

4. Mimi sitajua raha sawasawa,
Ila yote Yesu humpa,
Napata fadhili, na radhi kamili,
Niamini nitii pia.

5. Nitamfurahi, na kumtumai,
Nyumbani na mahali pote,
Agizo natenda, nikitumwa hwenda,
Niamini nitii pia.

NDIMI MFARIJI BASI

I'M A PILGRIM AND A STRANGER
NT 453 Whither pilgrim? OT 313 b Flat

106.

Ndimi msafiri basi, njia ni ya taabu,
Mashaka na wasiwasi, mambo yote Husibu,
Nikiona giza nyingi, mambo ya kusumbua,
Adui wakinichukiza, Yeye Baba ajua.

UONGOZI NA FARAJA

2. Na kila ninalowaza, mumu humu vitani,
Mateso yajapokaza, mimi hutumai,

Edit with WPS Office

Kweli nitafikia kule, mzigo nitautua,
Milele sitaushika, Yeye Baba ajua.

3. Daima ananitunza, Mwokozi ni Yesu tu,
Kwa kila haja hunifunza, mimi nikilenga juu,
Safari yangu ni ndefu, mwishowe nitapumua,
Kwake kwenye utukufu, yeye Baba ajua.

4. Mwokozi nikimwendea, huko juu kwa Mungu;
Sana nitamwabudu, ndiye mpenzi wangu,
Sitasumbuliwa tena, ndiko kwenye ukombozi,
Ni ahadi yake Bwana, Yeye Baba ajua.

NIMEHITAJI MWOKOZI

I MUST HAVE THE SAVIOUR

NT 376 I must have the Savior with me OT 640 E Flat

107.

Nimehitaji Mwokozi,
Awe name daima,
Nataka mikono yake,
Kunizunguka sana.

Hofu rohoni sina,
Aniongoze tena,
Sitanung'unika tena,
Nitamfuata daima.

UONGOZI NA FARAJA

2. Nimehitaji Mwokozi,
Sina lmani nyingi;
Atanifufua moyo,

Edit with WPS Office

Wengine hawawezi.

3. Nimehitaji Mwokozi,
   Mwendoni mwa maisha;
   Katika mateso mengi,
   Tena katika vita.

4. Nimehitaji Mwokozi,
   Kiongozi njiani,
   Kwa jicho aniongoze
   Nifike Mbinguni.

NI MIAKA MICHACHE

A FEW MORE YEARS SHALL ROLL

108.

Ni miaka michache,
Hivi ipitavyo,
Asipotokea Bwana,
Tutakwenda vivyo.

Nifanye tayari,
Osha dhambi zangu,
Nikubali siku ile,
Ee Bwana wangu.

2. Jua hili nalo,
   Siku chache tu,
   Na tutakwenda ambapo,
   Mwana ndiye nuru.

3. Ni vivyo ni chache,

Edit with WPS Office

Siku za tufani,
Hapana tufani kamwe,
Twendapo Mbinguni.

4. Ni kwa siku chache,
Kuachana kwetu;
Mashindano na machozi,
Hayako huko juu.

5. Kwa sabato chache,
Twafurahi sana,
Halafu sabato ndefu,
Pamoja na Bwana.

NI NA HAJA NAWE

I NEED THEE EVERY HOUR

NT 680 I need thee OT 479 A Flat

109.

Nina haja nawe,
Yesu Bwana,
Mwengine hawezi,
Kunifaa

Yesu, nakuhitaji,
Vivyo kila saa;
Niwezeshe, Mwokozi;
Nakujia.

UONGOZI NA FARAJA

2. Nina haja nawe,
Kaa name,
Majaribu haya,

Edit with WPS Office

Hayaumi.

3. Nina haja nawe,
   Kila hali,
   Maisha ni bure,
   Ukiwa mbali.

4. Nina haja nawe,
   Unifunze;
   Na ahadi zako,
   Nitimize.

5. Nina haja nawe,
   Mweza-yote,
   Ni wako kabisa,
   Siku zote.

UONGOZI NA FARAJA

NI ONAPO AMANI KAMA SHWARI

WHEN PEACE LIKE A RIVER.

Edit with WPS Office

NT 695 It is well with my soul OT 457 D Flat

110.

Nionapo amani kama shwari,
Au nionapo shida;
Kwa hali zote umenijulisha,
Ni salama rohoni mwangu.

Salama rohoni,
Ni salama rohoni mwangu,

2. Ingawa shetani atanitesa,
Nitajipa moyo kwani,
Kristo ameona unyonge wangu,
Amekufa kwa roho yangu.

3. Dhambi zangu zote, wala si nusu,
Zimewekwa msalabani;
Wala sichukui laana yake,
Ni salama rohoni mwangu.

UONGOZI NA FARAJA

NI ONGOZE BWANA MUNGU

GUIDE ME OH THOU GREAT JEHOVAH

NT 431 Calabar NT 414 Cwm Rhonnda OT 300 A Flat

Edit with WPS Office

111.

Niongoze Bwana Mungu,
Ni msafiri chini;
Ni mnyonge – nguvu sina,
Nishike mkononi;
Umkate wa Mbinguni,
Nilishe siku zote.

2. Kijito cha maji mema,
Kitokacho mwambani,
Nguzo yako, moto, wingu,
Yaongoza nyikani,
Niokoe mwenye nguvu,
Nguvu zangu na ngao.

3. Nikikaribia kufa,
Sichi neon lolote,
Wewe kifo umeshinda,
Unazo nguvu zote,
Tutaimba sifa zako,
Kwako juu milele.

UONGOZI NA FARAJA

SALAMA ILIYOTIMILIVU

PEACE, PERFECT PEACE
NT 516 Pax Tecum OT 674 C

Edit with WPS Office

112.

Salama, iliyo timilivu,
I wapi, na dunia ni mbovu?

2. Damu ya Yesu, ndiyo salama;
Ndiyo itwambiayo daima,

3. Salama, iliyo kamilifu,
Yote hapa, yana usumbufu.

4. Tufanyapo, apendayo Bwana,
Tutapata kwake rah asana.

5. Salama, iliyo timilivu,
Mengi machozi na maumivu.

6. Yesu ndiye, tabibu wa heri,
Umtegemeapo, ni shwari.

7. Si basi? Yesu yu nasi chini;
Punde aja, tupaza mbinguni.

8. Salama, nayo salama kweli,
Na wapenzi wetu, wako mbali?

9. Kwake twawekwa, sote salama;
Sisi na wao pia, wazima.

UONGOZI NA FARAJA

10. Salama, iliyo kamilifu;
Hatuoni mbele, tu vipofu.

Edit with WPS Office

11. Yesu yu mbele. hofu hapana,
Kwani twamjua, Yeye sana.

KWA MABAWA YA IMANI

GIVE ME THE WINGS OF FAITH TO RISE

NT 140 They'll sing a welcome home OT 89

113.

Kwa mabawa ya Imani,
Na nipae juu,
Kwao washinda, vitani,
Kwenye nuru kuu.

Wataniimbia wimbo,
Wanikaribishe huko,
Malaika pia,
Nikiwafikiria, watanikaribisha.

2. Walikua na kilio,
Tena masumbufu,
Mengi yawasumbuayo,
Dhambi, shaka, hofu.

UONGOZI NA FARAJA

3. Mishindaje hayo,
Kwa moja sauti,

Edit with WPS Office

Watajibu; ni kwa Kristo,
Na yake mauti.

4. Walimwandama hatua,
Kwa wampendavyo,
Mungu akawachukua,
Hata kwake vivyo.

UJARIBIWAPO USIFANYE DHAMBI

YIELD NOT TO TEMPTATION

NT 579 Yield not to temptation OT 333 A flat

114.

Ujaribiwapo, usifanye dhambi,
Bali uzishinde, kwa kumtii Yesu,
Fuliza kiume, ushinde tamaa,
Yesu ni Mwokozi, atakuokoa.

Umwombapo, Yu papo,
Akuongeze nguvu,.
Atakusaidia, Yesu atakufaa

UONGOZI NA FARAJA

2. Wepushe waovu, matusi, dharau,;
Heshima ya Mungu, kamwe sisahau,

Edit with WPS Office

Fanya uhodari, uwe mpole,
Atakuokoa hata milele.

3. Avumiliaye, hupewa taji;
Tujaposumbuka tu washindaji,
Na Mwokozi wetu, hutuwezesha,
Tusiwe kushindwa, kama twakesha.

UKIRUSHWA – RUSHWA NA DUNIA HII

WHEN UPON LIFE'S BILLOWS

NT 202 Count your blessings OT 592 E flat

115.

Ukirushwa – rushwa na dunia hii,
Utakapokufa moyo, kwa kudhii,
Zilivyo Baraka zihesabu tu,
Nawe utaona ni ajabu kuu.

Zilivyo Baraka zihesabu tu,
Mungu aliyofanya, ndiye makuu,
Zilivyo Baraka, zihesabu tu,
Nawe utaona, ni ajabu kuu.

UONGOZI NA FARAJA

2. Je, unalemewa na mzigo huu,
Msalaba wako ni mzito tu?

Edit with WPS Office

Hesabu Baraka, maisha yote,
Nawe utaimba, usikulemee.

3. Kwamba una mali, usifanye tamaa,
Yesu ndiye mali yako ya kufaa,
Hesabu Baraka, za chini na juu,
Hazinunuliki kwa thamani kuu.

4. Yatuumizayo, tutayasahau,
Na Baraka zetu, tusizidharau,
Hesabu Baraka, zisipotee,
Hesabu Baraka, hata uzoee.

5. Haya basi, ndugu, uende mbele tu,
Na usife moyo, Mungu ni mkuu,
Hesabu Baraka, nawe mngojee,
Hata mwisho atakua na wewe.

VITA

USIOGOPE MAADUI

Edit with WPS Office

GOD WILL TAKE CARE OF YOU

B Flat

116.

Usiogope maadui,
Atakulinda Yesu,
Katika mabawa ya Mungu,
Yesu, ni mlinzi.

2. Dhambi zote, uzikimbie,
Atakulinda Yesu,
Yakiwa mengi majaribu,
Yesu, ni mlinzi.

3. Ukipotewa na, ovyo vyote,
Atakulinda Yesu,
Hatayakataa maombi,
Yesu, ni mlinzi.

4. Unapoteswa na shetani,
Atakulinda Yesu,
M-tegemee, Bwana leo,
Yesu, ni Mlinzi.

VITA

Edit with WPS Office

WEWE TU MWENGI NE SI NA

ONLY THEE MY SOUL'S REDEEMER

OT 262 Only Thee A Flat

117.

Wewe tu, mwingine sina,
Mbinguni wala chini,
Mwenye kunitunza sana,
Kiongozi njiani.

Wewe tu, wewe tu,
Mpenzi, ni nawe tu.

2. Wewe tu, sioni tamu,
Ila furaha yako,
Ya kujua nitadumu,
Katika pendo lako.

3. Wewe tu, la, sitamani,
Sitamani vya watu,
Baraka za duniani,
Sizioni ni kitu.

4. Wewe tu, ni damu yako,
Iliyonitakasa,
Najitegemea kwako,
Yesu, tokea sasa

VITA

ASKARI WA YESU

Edit with WPS Office

118.

Askari wa Yesu,
Kale vitani,
Wenye ujasiri,
Wenye jina kuu,
Wali vumilia,
Hata kifoni,
Kumtumilikia, Kristo,
Msulubiwa.

Askari, Jeshini,
Askari, kweli,
Imani hodari,
Tunayo vitani,
Shaka tuondoe,
Kwa nguvu zake,
Fuata nyayo zake,
Vitani mwake.

2. Yesu kiongozi,
Jina tukufu,
Vita vyake tumo,
Uhuru twatangaza,
Kupinga shetani,
Tutasimama,
Mbele tutaenda,
Kwa Imanueli.

VITA

3. Tu askari wake,

Edit with WPS Office

Msalabani,
Vyake vita tumo,
Aibu haipo,
Wake ulimwengu,
Na mataifa,
Tutawaongoza,
Enzini mwake.

FURAHA, KUNA RAHA JESHI NI LA WOKOVU

JOY IN THE SALVATION ARMY

NT 706 Joy in the Salvation Army OT 390

119.

Furaha, kuna raha, Jeshini la wokovu,
Fu- ra- ha. Jeshini lake Bwana,
Imbeni, kwa Mungu, kwa sifa sauti kuu,
Sifuni, kwa ngoma, sifuni wokovu tuimbe,
Chezeni – ngoma, imba kwa raha,
Sifuni nyote, kwa sauti kuu,
Kwan chi ya ahadi twendayo,
Furaha kila saa.

Furaha, kuna raha,
Jeshini la wokovu,
Furaha, jeshini lake Bwana.

2. Furaha – kuna raha, Jeshini la Wokovu,
Furaha – Jeshini lake Bwana;
Damu – na moto – ni wito wa letu Jeshi,
Damu, na moto, ni ushindi wa vita.

VITA

Damu na moto, Vitani imba,
Damu ya moto, adui shinda,

Edit with WPS Office

Damu na moto, hutupa furaha,
Ushindi kila saa.

3. Furaha – kuna raha, Jeshini la wokovu,
Furaha – Jeshini, lake Bwana;
Twimbeni, twimbeni, dunia ijae shangwe,
Tupaze – sauti, anga ijae sifa,
Kwa tarumbeta na ngoma nyingi,
Tumsifu Bwana, nyumba za raha,
Tutaimba, hata Bwana arudi,
Tumsifu daima.

ASKARI WA MUNGU VITANI
GOD'S SOLDIER
NT 62

120.

Askari wa Mungu, vitani,
Askari aliye vitani,
Askari kweli, ambaye,
Atakusudia ya juu,
Askari huenda pa dhambi,
Vitani penye uovu,
Adui mjanja kushindwa,
Kwa kweli shetani kushindwa.

VITA

Twajaza utukufu duniani,
Twacheka na chuki hapana,

Edit with WPS Office

Na twaimba, hadithi ya injili,
Twageuza ulimwengu.

2. Askari wa Mungu, husimama pweke,
Mizigo ya wote, akubali,
Kazi pweke haepuki,
Pa giza na shida yupo,
Askari wa Mungu hodari,
Wajibu wake haachi,
Wengi wangoja wahitaji,
Mpango wa Mungu hapingi.

KRISTO WA DUNIA YOTE

CHRIST FOR THE WHOLE WIDE WORLD

NT 628 Christ for the whole wide world OT 698

121.

Waambie mashariki na magharibi,
Waambie ya umpendaye,
Jinsi ya kupumzika vyema,
Ukimtegemea Mwokozi,
Waambie yote ya Biblia,
Waambie kunayo maisha,
Bendera ikunjuliwe,
Kristo kwa dunia.

VITA

Waambie ya motto pale horini,

Edit with WPS Office

Kutoka Mbinguni,
Waambie ya alivyowafidia,
Kwa ajili ya pendo,
Waambie kwa neon na kwa vitendo,
Peperusha bendera,
Waambie kwa shangwe,
Waambie kwa shangwe,
Kristo kwa dunia.

2. Kwa ngoma za jeshi,
   Twatangaza,
   Kuwa Mwokozi dhambi kashinda,
   Waambie tajiri na maskini,
   Hadi nguvu zake wajue,
   Waambie watu wote pia.
   Kanisani pia njiani,
   Bendera ikunjuliwe,
   Kristo kwa dunia.

3. Waambie wazee na vijana,
   Kuwa mashujaa wa vitani,
   Waambie ya mlinzi na zizi,
   Tarumbeta navyo vinubi,
   Paza sauti ya kinubi,
   Eneza mbali na karibu,
   Bendera ikunjuliwe,
   Kristo kwa dunia.

VITA

DUNIA SHABAHA YETU

Edit with WPS Office

ALL THE WORLD
PT 277 A flat

122.

"Dunia", shabaha yetu,
Kusudi, letu pia,
Ni mavuno namna gani,
Tutavuna kwa Baba?

"Dunia" ko kote
Tutapata kwa Mungu,
Dunia ko kote,
Waokoke waaminifu.

2. "Dunia" kila taifa,
Lisikie Injili,
Wokovu na sifa zake,
Twishi nazo kamili.

3. "Dunia", na waijue,
Uhuru wa Mwokozi,
Fahari za ufalme wake,
Hazimo duniani.

4. "Dunia" iwe kwa Kristo,
Aliyetukomboa,
Askari kazeni mwendo,
Dunia kwake Mungu.

VITA

EE, SIKIZA, WEWE NAFSI YANGU

Edit with WPS Office

HARK, HARK MU SOUL
NT 548 Pilgrims OT E flat

123.

Ee, sikiza, wewe nafsi yangu,
Uelewe, nini ujumbe huu?
Huo ndio, sio wa ulimwengu,
Ni ujumbe, wenye furaha kuu;

Jeshi la wokovu,
Jeshi la Mungu,
Twende tushinde,
Kwa moto na damu.

2. Sikilizeni, ndio wajumbe wake,
Waletao ujumbe mwema huu;
Kila mtu amwendeaye kwake,
Atapata moyoni, raha kuu.

3. Ni sauti yake ipendezayo,
Sikizeni, mliolemewa;
Njoni kwangu, na ikulemeayo,
Nipe mimi, utasamehewa.

VITA

MLIO ASKARI

Edit with WPS Office

124.

Mlio askari,
Vaeni silaha,
Kaeni sana hodari,
Mbele kuna raha.

Haleluya, Haleluya, Haleluya,
Nasafishwa damini,
Nasafishwa damuni.

2. Ila saa vita,
Ni vita vikali,
Ila aliyewaita,
Yupo nanyi kweli.

3. Basi, simameni,
Muwe na Imani,
Mtazikanyaga chini,
Nguvu za shetani.

4. Atawapa nguvu,
Kesheni, ombeni,
Msiwe sasa na wivu,
Mkiwa vitani.

VITA

5. Mkiisha shinda,
Kwa nguvu za Bwana,

Edit with WPS Office

Kwake juu mtakwenda,
Kwa fahari sana.

MTETEENI YESU, MLI O ASKARI

STAND UP, STAND UP FOR JESUS

NT 264 Stand up for Jesus OT 183 B flat

125.

Mteteeni Yesu, mlio askari,
Inueni beramu, make tayari,
Kwenda naye vitani, sisi hatuchoki,
Hata washindwe pia, yeye amiliki.

2. Mteteeni Yesu, vita ni vikali,
Leo siku ya Bwana, atashinda kweli,
Waume twende naye, adui ni wengi,
Lakini kwake Bwana, tuna nguvu nyingi.

3. Mteteeni Yesu, ,mwenye ushujaa,
Nguvu zenu za mwili, hazitatufaa;
Silaha ya injili, vaeni daima.

4. Mteteeni Yesu, vita ni vikali,
Wengi wamdharau, hawamkubali,
Ila atamiliki, tusitie shaka,
Kuwa naye vitani, twashinda hakika.

VI TA

MUNGU NI KI ONGOZI WETU

GOD I S KEEPI NG HI S SOLDI ERS FI GHTI NG

Edit with WPS Office

126.

Mungu ni, kiongozi wetu,
Tu askari zake wa kweli,
Mashetani wanapotupinga,
Hakika tutawashinda,
Kushinda amejaribu,
Bali bendera yetu,
Huleweshwa kwa nguvu zote,
Kwani hatutashindwa.

La, hatutashindwa,
Kabisa, kabisa, kabisa,
La, sisi hatutashindwa kabisa,
Tunala kusudi kushinda daima.

2. Tutamwandama, Yesu Bwana,
Wafukuzwe adui wote,
Vikosi vyetu havisiti,
Watashinda ama kufa,
Haki, Utakatifu,
Wokovu, wimbo wetu,
Tutasimama daima,
Kwani hatutashundwa.

VITA

3. Wokovu kwa watu wote,
Twenenda dunia popote.

Edit with WPS Office

Nguvu za kuokoa wote,
Msalabani mwake;
Tutashinda kabisa,
Uovu na shetani,
Washinda kwa milele,
Kwani hatutashindwa.

NA TUIMBE DAIMA

MAKE THE WORLD WITH MUSIC RING
NT 768 Over Jordan OT 498 E flat

127.

Na tuimbe daima,
Jina la Yesu Bwana,
Tutamtukuza sana, Haleluya!
Waambie watu wote,
Wa dunia popote,
Yesu, Mweza-wa-Yote, Haleluya!

Haleluya, Haleluya,
Na tushinde kwa damu,
Tutamtukuza Mungu,
Haleluya, Haleluya,
Na tushinde kwa damu,
Haleluya!

VITA

2. Kwa damu tutashinda,
Shetani na dunia,

Edit with WPS Office

Mungu hutuwezesha, Haleluya;
Tujiweke tayari,
Kupigana vitani,
Kwetu hatushindiki, Haleluya!

3. Kwa uwezo wa Bwana,
Siku zote kutosha,
Adui kufukuza, Haleluya!
Twende mbele dawamu,
Kwa Yesu Bwana wetu,
Tumaini ni letu, Haleluya!

4. Imbeni, watu wote,
Tutakwenda juu sote,
Mbinguni kwa milele, Haleluya!
Usoni tutaona,
Yesu aliyekufa,
Kutuokoa kabisa, Haleluya!

NCHI ZOTE, GARI LA WOKOVU

ALL ROUND THE WORLD

NT 769 Poor Old Joe OT 326 D

128.

Nchi zote, gari la wokovu,
Lazunguka, Bwana huokoa,
Bendera ya Jeshi la WOkovu,
Muiinue askari bila hofu.

VITA

Lewesheni, lewesheni,

Edit with WPS Office

Bendera iwe juu,
Na ileweshwe basi,
Kwa fahari kuu.

2. Nchi zote kwa nyimbo na mbiu,
Tutakwenda na bendera yetu,
Kutangaza jina lake Yesu,
Na kuinua bendera ya wokovu.

3. Mkombozi damu alimwaga,
Kuokoa nchi zote sasa,
Sisi hapa tu askari wake,
Tutakwenda vitani pamoja naye.

NI MASHUJAA WENGI

I HAVE READ OF MEN OF FAITH

NT 651 Girdon the amour OT 463 A Flat

129.

Ni mashujaa wengi,
Wenye nguvu Imani,
Wameshinda huko vitani,
Nasikia kuitwa,
Niwe askari sasa,
Niwfuate wa zamani.

VITA

Navika mavazi, ya kupigana,
Kusudi kushinda, si kukimbia,

Edit with WPS Office

Adui na waj ue,
Hapa mahali pot e,
Mimi askar i wa Yehova.

2. Mimi nit asimama,
Kwa Mungu, wangu Bwana,
Kuwa na panga mkononi,
Nit avikwa na t aj i,
Kwa wale washindaj i,
Kwa milele huko mbinguni.

3. Mimi nit apigana,
Kwa uwezo wa Bwana,
Yeye ni Mweza wa yot e,
Sit or oki vit ani,
Penye hat ar i kuf a,
Hat a shet ani na ashindwe.

4. Wewe umesikia,
Mwit o wa kupigana,
Uwe Askar i mwenye haki;
Yesu akuit a sasa,
Kupigana daima,
Kushinda kabisa shet ani.

VI TA

NI NANI ATAPI GANA

Edit with WPS Office

WHO'LL FIGHT FOR THE LORD?

NT 483 The home over there NT 484 We speak of the realms OT 210 C

130.

Ni nani atapigana,
Kwa Bwana, hapa dawamu;
Hata tuonane daima,
Mbinguni kwake huko juu?

Kwa Bwana, popote;
Ni nani atapigana?
Kwa Bwana, popote,
Ni nani atapigana?

2. Si kutaka enzi, wala heshima,
Tuingiavyo salfu, ya Yesu Mwema,
Ila ni mapenzi, yatuvutayo,
Amwitaye Bwana, ni wake huyo.

3. Alitununua, 'Si kwa dhahabu;
Thamani ni damu, ndiyo ajabu;
Kristo, utujaze Roho wa nuru,
Nasi tu tayari, 'uhuru wetu.

VITA

NI NANI WA BWANA

Edit with WPS Office

WHO IS ON THE LORD'S SIDE?

NT 200 Armageddon NT 207 Rachie OT 383 G

131.

Ni nani wa Bwana, ni kina nani?
Watu wataka okwenda vitani?
Nani atakayevuta wenziwe?
Waje wokovuni, wasipotee?

Wako ukombozi, yako neema,
Tu upande wako, Bwana, daima.

2. Si kutaka enzi, wala heshima,
Tuingiavyo safu, ya Yesu Mwema,
Ila ni mapenzi, yatuvutayo,
Amwitaye Bwana, ni wake huyo.

3. Alitununua, 'si kwa dhahabu;
Thamani ni damu, ndiyo ajabu;
Kristo, utujaze Roho wa nuru,
Nasi tu tayari, 'uhuru wetu.

4. Vita ni vikali, hatutaona,
Mwenye kulishinda jeshi la Bwana,
Chini ya bendera tumesimama,
Ndiko kushindia, ndiyo salama

VITA

NJOONI SASA, TUINGIE JESHI

COME, JOIN OUR ARMY

Edit with WPS Office

132.

Njooni sasa, tuingie Jeshi,
Yesu yu nasi, na tupigane,
Tetea haki, kishinda dhambi,
Kwani Jeshi la Wokovu, laenda mbele.

Laenda mbele, laenda mbele,
Jeshi la wokovu, laenda mbele,
Askari wa Yesu, mwe hodari,
Kwani jeshi la Wokovu, laenda mbele

2. Njooni, tumfukuze shetani,
Yesu Bwana, ndiye kiongozi,
Vita vikali, hebu tushinde,
Kwani Jeshi la Wokovu, laenda mbele.

3. Njooni sasa, tusiwe hofu,
Watu wa kweli, sasa dawamu,
Wokovu wake, ni wimbo wetu,
Kwani Jeshi la Wokovu, laenda mbele.

VITA

PIGA KELELE!
SOUND THE BATTLE CRY

Edit with WPS Office

133.

Piga kelele,
Adui yule,
Bendera shika,
Kwa Bwana;
Vaa silaha,
Yenye imara,
Litegemee neno lake.

Zindukeni, askari wa Jeshi,
Enezeni, neon la Mungu;
Twende mbele tuimbe hosana,
Kapiteni ni, Bwana Yesu.

2. Tuwe hodari,
Tukisafiri,
Juu ya adui,
Tushinde;
Silaha zetu,
Zing'are kwetu,
Na tushinde,
Tusianguke.

VITA

3. Mungu wa wote,
Kwa sisi sote,

Edit with WPS Office

Utusikie,
Na neema;
Mwisho vitani,
Kwa duniani,
Tuvae taji,
Mbele yako.

PIGA SANA VITA VYEMA

FIGHT THE GOOD FIGHT

NT 40 Pentecost NT 17 Duke Street OT 4 G

134.

Piga sana vita vyema,
Kwa ushujaa daima,
Yesu ndiye nguvu zako,
Yesu ndiye kweli wako.

2. Kaza mwendo, ushindane,
Tazama mbele, si nyuma;
Ni yeye, Uzima wako,
Naye ni mpenzi wako.

3. Changamka, uamini,
Akushika mikononi,
Hageuki, akupenda,
Kuwa naye una raha.

VITA

TU ASKARI WA BWANA, PIGANIE

Edit with WPS Office

SOLDIERS FIGHTING ROUND THE CROSS

NT 600 All hail, I'm saved! OT 444 B Flat

135.

Tu askari wa Bwana, pigane,
Zunguka msalaba, piganie.

Haleluya, naokoka,
Njooni na muingie Jeshi,
Hapa, sasa, tutashinda kweli.

2. Futa panga kwa Bwana, piganie,
   Adui kufukuza, Piganie.

3. Kristo ndiye Rafiki, Piganie,
   Sisi hatutashiundwa, Piganie.

4. Piga vita, amini, piganie,
   Tutashinda halisi, Piganie.

5. Uwe mwaminifu, piganie,
   Mtumishi dawamu, Piganie.

6. Nyara kuona juu, Piganioe,
   Kwako wewe juu mbingu, Piganie.

7. Usijikimbilie, Piganie,
   Simama utashinda, Piganie.

VITA

Edit with WPS Office

TWENDE MBELE, TUPIGANE

TO THE FRONT, THE CRY IS RINGING

NT 841 Victory for me OT 384 G

136.

Twende mbele, tupigane,
Twende mbele vitani,
Mashujaa wameitwa,
Wenye nguvu, Imani;
Hatutayatafuta,
Yale ya kutuzuia'
Hofu na hushundika,
Mungu atatuwezesha.

Tusirudi, na tushinde,
Tuko pamoja;
Mungu atatutazama,
Tutashinda, tutashinda,
Kwa damu ya Bwana Yesu,
Kushinda kwetu,
Kwa yake Damu.

2. Twende mbele pa vitani,
Kristo hutuongoza,
Nguvu zetu na Imani,
Ziko kwake Mwokozi,
Tumekisikiliza,
Kilio cha wenye dhambi;
Bwana ameamrisha,
Twende waletwe zizini.

VITA

3. Twende na usikawie,
Wengi hufa dhambini,

Edit with WPS Office

Twende mbele tumfuate,
Bwana, mwenye mapenzi;
Wakosaji gizani,
Watumwa wa mashetani,
Wangoje, tuwaletee,
Wokovu, Raha, Amani.

TU KUNDI KUSHINDA ADUI

WE'RE A BAND THAT SHALL CONQUER

NT 508 We shall win OT 321 A Flat

137.

Tu kundi kushinda adui,
Tukiwa na nguvu za Bwana;
Na tuwe askari wa kweli,
Watu wake Yesu kuleta.

Amini! Tushinde!
Tukiwa na nguvu za Bwana,
Amini! Tushinde!
Tukiwa na nguvu za Bwana.

2. Adui ndio wengi kweli,
Na vita ndivyo ni vikali,
Ila Bwana "Mweza – wa – yote".
Tutashinda tukiwa naye.

VITA

3. Tumeshinda zamani kale,
Na kuwafukuza adui;

Edit with WPS Office

Tupigane kwa jina lake,
Silaha za injili tuvae.

4. Tuwe waaminifu sasa,
Kwa Mungu na kwa jeshi pia;
Tushinde kwa moto wa damu,
Kuuokoa ulimwengu.

TUTUME TUTTUME, MUNGU NA TUTUME

TO THE WAR!

NT 557 Fighting on OT 341

138.

Tutume, tutume, Mungu na tutume,
Tutume kwa vita vilivyo vikali;
Kila kazi tufanye kwa nguvu yetu,
Ambayo tumepewa na Bwana wetu.

Kwa bidii, kwa bidii,
Kwa bidii, kwa bidii,
Tukeshe tuombe,
Tufanye hata aje Bwana.

2. Tutume, tutume, wenye njaa walishwe,
Maji ya uzimawa kiu wanyeshwe;
Ile giza na dhambi zote zikome,
Tushukuru kwa kuwa neema ni bure:

VITA

3. Tutume, tutume, Mungu na tutume,
Msifuni Kristo aliyetufia,

Edit with WPS Office

Ile bendera yetu ya rangi tatu,
Iwahubiri wote, 'Neema ni bure'.

4. Tutume, tutume, Mungu na tutume,
Kisha tutavikwa mavazi meupe,
Watakatifu kama jua watang'aa,
Tutaimba pamoja, 'Neema ni bure'.

TWAENDA MBELE NA NGAO UPANGA

WE ARE MATCHING ON WITH THE SHIELD

NT 661 Happy song OT 462 A Flat

139.

Twaenda mbele na ngao, upanga,
Kwa Mungu na tupigane daima;
Tutamsifu na kumtukuza sana,
Hata aje Yesu Bwana.

Amkeni, amkeni, salama, salama
Sifuni, sifuni, tukienda mbeleni,
Na tuimbe kwa jina lake Bwana,
Kwa nchi aliyotuahidia,
Njooni nyote tuwe askari zake,
Hata aje Yesu Bwana.

VITA

2. Mahali pote tu Jeshi la Bwana,
Tuleweshe juu bendera letu;

Edit with WPS Office

Msalaba wake tutajitwika,
Hata aje Yesu Bwana.

3. Twanenda mbele, Bwana yupo hapa,
Atalinda, kuongoza daima;
Adui wakija, tutawafukuza,
Hata aje Yesu Bwana.

4. Twanenda mbele, tutawasili juu,
Tutavikwa taji, na furaha kuu;
Wala hazitakoma sifa zetu,
Hata aje Yesu Bwana.

ASKARI SHUJAA KWENDA VITANI

KEEP IN STEP

NT 707 Keep in step

140.

Askari shujaa kwenda vitani,
Andama kila saa;
Usichelewe wala kusita,
Andama kila saa;
Pengine njia ndefu ngumu,
Hatari nyingi zahofisha,
Usishindwe vumilia,
Na andama kila saa.

VITA

Andama kila saa,
Andama kila saa,

Edit with WPS Office

Usichoke na kupumzika,
Kwa furaha mfuate Yesu,
Andama kila saa,
Andama kila saa,
Utaona njia ni rahisi,
Ukiandama kila saa.

2. Askari shujaa usife moyo,
Andama kila saa;
Mfuate Yesu popote,
Andama kila saa;
Vitani nenda kwa ushujaa,
Usishindwe kwa mapambano,
Mwamini Yesu, ni ngao, kiongozi,
Hivyo andama kila saa.

3. Askari shujaa, piga vita,
Andama kila saa;
Vaa silaha, ngao chukua,
Andama kila saa;
Mbele, mbele, amri ya Bwana,
Penye haki sasa simama,
Nenda mbele nchi ya ahadi,
Na andama kila saa.

VITA

TWENDENI ASKARI WATU WA MUNGU

ONWARD CHRISTIAN SOLDIERS

NT 205 Onward, Christian soldiers NT 200 Armagedon OT E Flat

Edit with WPS Office

141.

Twendeni askari, watu wa Mungu,
Yesu yuko mbele, tumwandame juu,
Ametangulia, Bwana vutani,
Twende mbele kwani ndiye amini,
Twendeni askari,
Kimasihia,
Yesu yuko mbele,
Tumwandame juu.

2. Jeshi la shetani, likisikia,
Jina la Mwokozi, litakimbia,
Kelele za shangwe, zivume nchi,
Ndugu, inueni, zenu sauti;
Na twende askari,
Kimasihia,
Yesu yuko mbele,
Twamwandamia.

3. Kweli kundi dogo, watu wa Mungu,
La mababa yetu, ni letu fungu;
Hatutengwi nao, moja Imani,
Tumaini moja, na moja dini;
Na twende askari,
Kimasihia,
Yesu yuko mbele,
Twamwandamia.

UTAKATI FU NA UTUMI SHI

4. Haya mbele watu, nasi njiani,
Inueni mioyo, nanyi sifuni;
Heshima na sifa, ni ya mfalme,
Juu hata chini, sana zivume;

Edit with WPS Office

Na twende askari,
Kimasihia,
Yesu yuko mbele,
Twamwandamia.

BWANA ASEMA, NI MTUMI E NANI
THE LORD SAYS, WHOM SHALL I SEND

142.

Bwana asema, nimtume nani,
Na ni nani atakayekwenda, badala yangu,
Na ni nani atakayekwenda, badala yangu,

Nitume mimi Bwana,
Nitume mimi Bwana,
Nitume mimi Bwana,
Nitume mimi Bwana.

2. Ninaogopa umri mdogo,
Kuhubiri neon lake Bwana, huko niendako,
Kuhubiri neon lake Bwana huko niendako.

UTAKATI FU NA UTUMI SHI

3. Midomo yangu, michafu sana,
Uichome kwa kaa la moto, uitakase,
Uichome kwa kaa la moto, uitakase.

Edit with WPS Office

4. Aliniambia nisiogope,
Nitapata ujasiri mwingi, kutoka kwake,
Nitapata ujasiri mwingi, kutoka kwake.

MWOKOZI ATAFUTA KUOKOA

THE SAVIOR OF MEN

NT 540 The old rustic bridge OT 494

143.

Mwokozi atafuta kuokoa,
Mioyo iliyopotea,
Alivutiwa dunia kupenda,
Kwa huruma yake tele,
Watenda kazi, bado ni wachache,
Na wenye njaa, pia wapo,
Wenye kulia, katika giza kuu,
Wanao taka kuongozwa.

Nisipovutiwa na huruma,
Roho wako hayupo nami,
Kunena, kutenda,
Nahitaji pendo,
Najua wewe mpaji.

UTAKATIFU NA UTUMISHI

2. Ndiye Kristo kati ya watu leo,
Kilio chao hakiishi,
Atawaonyesha, wanaopenda,
Kujua mambo ya amani;

Edit with WPS Office

Bila mhubiri wa juaje;
Wala juhudi za huruma,
Watavutwaje, pendoni mwa Bwana;
Bila mhuri wa Baraka.

3. Haki kwa nguvu, haitafanyika,
Wala werevu, kupumzika;
Kwa nia huoni, tamaa ya moyo,
Wala kuwatuliza watu;
Mwokozi wa watu niguze,
Mtumishi wako na awe,
Na mkazo kutumika na kuomba,
Kwa papo daima kwako.

BWANA NI KIJI KWAA

SAVIOUR IF MY FEET HAVE FALTERED

NT 370 Face to Face NT 449 The vacant chair OT 318

144.

Bwana nikijikwaa,
Njia ya msalabani;
Kibadilika kusudi,
Wema kutatizika,
Usinizuie kazi,
Nizidi kutumika;
Nioshe kikamilifu,
Nitakufurahia.

UTAKATIFU NA UTUMISHI

Yote kazi ni ya Bwana,
Ndiye yangu tamaa;
Niwe mwaminifu kwake,

Edit with WPS Office

Ninapojaribiwa.

2. Ninatumika kwa ujira,
Au kuweka nadhiri;
Kwa moyo ulio na pendo,
Maisha kuokoa;
Bwana wayajua yote,
Nalo kusudi ndilo,
Hukumu kuisubiri;
Ya wako usingizi.

3. Litwae pendo lako,
Nalo libubujike;
Ndani ya moyo wangu,
Kazi yanguifae;
Pendo la kuvumilia,
Pendo lenye chimbuko,
Lenye moyo na dhamira;
Kristo humtumika.

MBELE YAKE MWOKOZI WANGU
MUST I GO EMPTY HANDED

145.

Mbele yake Mwokozi wangu,
Je, nisimame maskini,
Sina cha kum- tumikia,
Cha kumpa sinacho,

UTAKATIFU NA UTUMISHI

Nisimame mbele ya Mungu,
Sina kitu cha kumpa;
Bila hata na tunda moja,
Je, nisimame hivyo?

Edit with WPS Office

2. Siku nyingi nilizitupa,
Zingerudi siku zile,
Ningempa Mwokozi wangu,
Ningemtumikia.

3. Ndugu yangu, amka leo,
Bwana bado akuita,
Kifoni hunayo nafasi,
Ya kumtumikia.

4. Nisimame mbele ya Mungu,
Sina kitu cha kum- pa,
Bila hata tu tunda moja,
Je, utakua hivyo.

MOTO, MOTO, UNAWAKA

BURNING, BURNING

NT 364 Burning, Burning

146.

Moto wa utakatifu,
Moto wa utakaso,
Yatimizwe 'matumaini'
Ndani ya moyo wangu.

UTAKATIFU NA UTUMISHI

Moto, moto, unawake,
Nitakaswe kabisa,
Nafua kusudi lako,
Nalo ni langu pia

Edit with WPS Office

2. Moto, moto unawake,
Kusafisha kabisa,
Napokea pendo lako,
Lifanye kazi yako.

3. Moto, moto, unawake,
Mungu roho kaa name,
Kama utakavyo wewe,
Ndiyo nataka mimi.

BWANA ULI NI PENDA

MY LORD LOVED ME

OT 178 Holy Spirit, faithful Guide G

147.

Bwana ulinipenda,
Nilipotanga – tanga;
Uniongoze, Bwana,
Safari ya maisha.

Ni wako, Ewe Bwana,
Najitoa maisha,
Unitumie sana,
Uwe wa kutukuzwa.

UTAKATIFU NA UTUMISHI

2. Bwana, maneno yako,
Na yawe nuru kwangu,
Fimbo na gongo lako,
Ni tegemeo langu.

Edit with WPS Office

3. Niletee Roho yako,
Ujaze moyo wangu,
Huko mbinguni kwako,
Ndiko makao yangu.

4. Bwana, mapenzi yako,
Kwako yamenileta,
Na kwa uwezo wako,
Daima nitashinda.

BWANA YESU NATAMANI

PRECIOUS JESUS, O TO LOVE THEE
NT 368 Denmark Hill NT 372 Glory to the Lamb OT 287 A Flat

148.

Bwana Yesu natamani,
Nakupenda uwe wangu,
Najitoa yangu nafsi,
Ukiifanya yako.

Enzi yake, haleluya,
Enzi yake kondoo;
Damu yanifikilia,
Enzi yake kondoo.

UTAKATIFU NA UTUMISHI

2. Twaa pendo, nalo haba,
Twaa akili na nia,
Lete Roho mtakatifu,
Nijaze moyo wangu

Edit with WPS Office

3. Nagusa mavazi yako,
Kwa mkono wa Imani,
Nawe uniponye name,
Na umri wa mapenzi.

4. Pendo ninalo rohoni,
Lenye thamani sana;
Limefanywa, likasemwa,
"Uwe safi kabisa".

5. Kweli, ni kiumbe kipya,
Nainuka mtakatifu;
Moyo umefufuliwa,
Ni wake, Yeye wangu.

CHINI YA MSALABA

BENEATH THE CROSS OF JESUS

NT 618 Beneath the cross OT E Flat

149.

Chini ya msalaba,
Nataka kuwako,
Ndio mwamba safarini,
Wa kivuli chema;
Ni kweli roho yangu,
Ni tuo kamili,
Kutua mzigo wangu,
Jua likiwa kali.

UTAKATIFU NA UTUMISHI

2. Na Yesu msalabani,
Walimkemea,
Alikufa niokoke,
Niliyepotea,
Naona ajabu sana,

Edit with WPS Office

Ya mambo mawili,
Jinsi anavyonipenda,
Nisiyestahili.

3. Atakayeonana,
Na Yesu mbinguni,
Njia yake aanzapo,
Ni msalabani;
Wokovu upo hapo tu,
Mwengine hapana,
Kisha kuna raha kuu,
Pamoja na Bwana.

EE YESU BWANA, NI WE MTAKATIFU

LORD JESUS, I LONG TO BE

NT 556 Cossar NT 563 Lord Jesus I long OT 344 A Flat

150.

Ee Yesu Bwana, niwe mtakatifu,
Uishi kwangu, sasa na dawamu,
Ondoa pepo, adui fukuza,
Unitakase, ni safi kabisa,

Niwe safi, naam; safi sasa,
Unitakase, ni safi kabisa.

UTAKATIFU NA UTUMISHI

2. Ee Yesu Bwana, isibaki kwangu,
Alama zote, za dhambi zangu,
Ziondoe zote, kwa damu yako,
Unitakase, ni safi kabisa,

Edit with WPS Office

3. Ee Yesu Bwana, uje kwangu chini,
Nisaidie, nijitoe kweli,
Nakupa moyo na maisha yote,
Unitakase, ni safi kabisa.

4. Ee Yesu Bwana, Unione hapa,
Na uje kwangu, Uniumbe tena;
Kwa wafuatao, hajawakataa,
Unitakase, niwe safi kabisa.

5. Ee Yesu Bwana, ninayo Baraka,
Umenisafisha, nimetakasika,
Maombi yashinda, sasa najua,
Nimesafishwa, na damu kabisa.

IFUFUE KAZI

REVIVE THY WORK, O LORD

NT 185 Pease NT 183 For ever with the Lord OT 140 A Flat

151.

Ifufue kazi,
Unyoshe mkono,
Itoe sauti kubwa,
Utuamshe mno.

UTAKATIFU NA UTUMISHI

Ifufue kazi,
Hapa twakuishi,
Tuna haja nawe, Bwana,
Tushukie sasa.

Edit with WPS Office

2. I fufue kazi,
Nasi tufufuke,
Moto wa Roho moyoni,
Sana na uwake.

3. I fufue kazi,
Tutilie kiu,
Na njaa ya haki yako,
Kwa Roho wa juu.

4. I fufue kazi,
Ujikuze jina;
Bwana tia pendo nyingi,
Tuwe kupendana.

5. I fufue kazi,
Nyesha mvua kwetu;
Sifa, Bwana, twae Wewe,
Baraka ni yetu.

UTAKATIFU NA UTUMISHI

KONDOO WA KALWARI

BLESSED LAMB OF CALVARY

NT 315 Spanish Chant NT 298 Thou art a mighty Saviour OT 149 B Flat

Edit with WPS Office

152.

Kondoo wa Kalvari,
Roho yako nzuri,
Nije nisafishwe,
Kwa neon neon lako Wewe,
Ili maisha yangu,
Yakutukuze Mungu.

2. Teketeza moyoni,
Dhana za mambo duni,
Liwake pendo langu,
Kwa mwanga wa Mungu,
Ili kwa watu niwe,
Kushuhudia Wewe.

3. Nifundishe kusinda,
Makosa na hatia,
Nipe huruma yako,
Kwa wakengeukao,
Ili nishuhudiwe,
Ninakupenda Wewe.

UTAKATIFU NA UTUMISHI

KRISTO! MWAKO WA KUSAFISHA

THOU CHRIST OF BURNING, CLEANSING FLAME

NT 335 Tucker OT 234 F

Edit with WPS Office

153.

Kristo! Mwako wa kusafisha,
Tulete e moto mioyoni,
Twataka kutakaswa sana,
Tulete e mioto mioyoni;
Tazama kundi la kudumu,
Tupe Roho mtakatifu,
Pentekote na ije kwetu,
Tulete e moto mioyoni.

2. Mungu wa Eliya, sikia,
Tulete e moto mioyoni;
Tuwezeshe ishi au kufa,
Tulete e moto mioyoni,
Dhambi zote kuteketeza,
Nuru 'tukufu' ingiza,
Ugeuzo sana kuanza,
Tulete e moto mioyoni.

3. Ni moyo tunaoulilia,
Tulete e moto mioyoni,
Utatimiza haja zetu,
Kwa nguvu za kufanya haki,
Neema kushinda vitani,
Uwezo ili tuwe safi,
Tulete e moto mioyoni.

UTAKATIFU NA UTUMISHI

4. Kuthibitisha mioyo yetu,
Tulete e moto mioyoni;
Watu wote waokolewe,

Edit with WPS Office

Tulet ee mot o mioyoni;
Mat habahuni t waj iweka,
Vyot e, uhai, maisha,
Sasa, kwa kuvikamilisha,
Tulet ee mot o mioyoni.

KWA DAMU YA KONDOO ALI YEKUFA

LORD THROUGH THE BLOOD OF THE LAMB

NT 512 Cleansing for me NT 513 Long, long ago OT 400 G

154.

Kwa damu ya kondoo,
Niwe safi, niwe safi;
Kwa hukumu ya makosa yangu,
Niwe safi, niwe safi,
Dhambi na giza vimenifunga,
Kwa siku zot e zimenishinda,
I la sasa, namwamini Bwana,
Niwe safi, niwe safi;

2. Kwa kilio cha makosa yangu,
Niwe safi, niwe safi;
Yaondolewe na damu sasa,
Niwe safi, niwe safi;
Yesu naliamini neon lako,
Unikubali nikij a kwako,
Kwa dhambi nisiwe na maj ut o,
Niwe safi, niwe safi.

UTAKATI FU NA UTUMI SHI

3. Kwa mashaka ya kuhuzunisha,
Niwe safi, niwe safi,
Kwa hofu za kunihukumisha,

Edit with WPS Office

Niwe safi, niwe safi,
Yesu, sijafahamu maana bado
Kwa Imani nanyosha mkono,
Nisimame kwa neema yako,
Niwe safi, niwe safi.

4. Kwa hofu, zote za wanadumu,
Niwe safi, niwe safi,
Nisiogope kushuhudia,
Niwe safi, niwe safi.
Bwana, nizidishie nguvu zako,
Niwe daima mjumbe wako,
Nikionjwa niimbe wimbo,
Niwe safi, niwe safi.

LOO KWAMBA NI PATE MOYO SAFI

O FOR A HEART THAT IS WHITER
NT 528 O for a heart whiter than snow OT 397 D

155.

Loo, kwamba nipate moyo safi,
Kuweka daima damuni mwake;
Nitakaswe nisiwe na dhambi,
Niwe na Yesu wangu Mwokozi,

UTAKATIFU NA UTUMISHI

Safi moyo, safi moyo,
Mwokozi mwema nalia kwako,
Ulijitoa kwa mapenzi makuu,
Leo nitakase moyo wangu.

Edit with WPS Office

2. Loo, kwamba nipate moyo safi,
Nipe moyo kujazwa amani,
Kuburudishwa umande wa mbingu,
Nimtumikie kwa nguvu yangu.

3. Loo, kwamba nipate moyo safi,
Mwali wa Roho kuwaka ndani,
Nijaze pendo lililo na nguvu,
Liuondoe uchafu wangu.

4. Loo, kwamba nipate moyo safi,
Ndipo kukua kwa neema yake,
Nifanane na mfano wake,
Hata niuone uzuri wake.

NASIKIA KUITWA

I HEAR THY WELCOME VOICE

NT 169 I hear thy welcome voice OT 137 D

156.

Nasikia kuitwa,
Na sauti yako,
Unisafishe kwa damu,
Ya kuangikwa kwako.

UTAKATIFU NA UTUMISHI

Nimesongea mtini pako.
Nisafishe kwa damu,
Ya kuangikwa kwako.

Edit with WPS Office

2. Ni mnyonge kweli,
Umenipa nguvu,
Nawe umenitakasa,
Kwa utimilivu.

3. Yesu hunifunza,
Mapenzi, Imani,
Tumai, amani, radhi,
Hapa na mbinguni.

4. Huishuhudia
Mioyo ya Imani,
Ya kuzipata ahadi,
Kwa kumwamini.

NI MEAHI DI , YESU

O JESUS, I HAVE PROMI SED

NT 248 Day of rest NT 246 Aurelia OT 189 E Flat

157.

Nimeahidi, Yesu,
Kukutumikia,
Wewe U Bwana wangu,
U rafiki pia;
Sitaogopa vita,
Wewe U Mwokozi;
Nisiiache njia,
Ee Kiongozi.

UTAKATI FU NA UTUMI SHI

2. Yesu uwe karibu,
Kuliko dunia,
Ya majaribu yake,
Mengi nasikia,
Kuliko na adui,

Edit with WPS Office

Nje na kwa ndani,
Nivute Ee Bwana.
Kwako ubavuni.

3. Nikusikie Wewe,
Nena name, Bwana;
Kelele za dunia,
Ndizo nyingi sana,
Nena, kunihimiza,
Au kunionya;
Nena, nikusikie,
Mwenye kuniponya.

4. Umewapa ahadi,
Wakafuatao,
Kwenda uliko Wewe,
Wawe kuko nao;
Nami nimeahidi,
Kukutumikia,
Nipe neema, Bwana,
Kukuandamia.

5. Hatua zako Bwana,
Na nizikanyage,
Wewe u Mwenye nguvu,
Mimi ni mnyonge;
Niongoze, nivute,
Nishike daima,

UTAKATIFU NA UTUMISHI

Mwishoni niwasili,
Mbinguni salama.

TAFUTA DAIMA UTAKATIFU
TAKE TIME TO BE HOLY

Edit with WPS Office

NT 571 Take time to be holy OT 685 F

158.

Tafuta daima utakatifu,
Fanya urafiki na wakristo tu;
